**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
# WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

Simu: +255262963470
Barua Pepe: ps@mit.go.tz
Barua Pepe: gcu@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz
Nukushi: +255262963117

Mji wa Serikali, Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S.L.P 2996,
**40478, Dodoma**.

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA TBS

**29 Juni, 2021, DODOMA.**

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Prof. Kitila A. Mkumbo (Mb.), kwa mamlaka aliyo nayo kwa mujibu wa **Sheria ya Viwango, 2009**, hususani **Kifungu cha 5 (2)** ameteua Wajumbe kumi (10) wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dkt. Fenella Ephraim Mukangara, Mhadhiri Mwandamizi Mstaafu, kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliteuliwa na Mamlaka husika tarehe 19 Juni 2021.

Wajumbe walioteuliwa na Mhe. Prof Mkumbo ni kama ifuatavyo:

1. Bw. Twalib Timoth Mmbaga kutokaTaasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF);
2. Bw. Kalumuna Prosper Benedicto kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Tanzania (SIDO);
3. Dkt. Nandera Ernest Mhando kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM);
4. Bw. Robert Pelegrine Mtengule kutoka Wizara ya Fedha na Mipango;
5. Dkt. Catherine Camite Joachim kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto;
6. Bi. Aneth Jackson Mathania kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara;
7. Bw. Shaban Ahamed Kabunge kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
8. Bi. Magdalena Ludovick Utouh kutoka Tume ya Ushindani (FCC);
9. Dkt. Eliapenda Elisante Mariki kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA); na
10. Bw. Hussein Suphian Ally kutoka Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI)

Uteuzi wa Wajumbe hao unaanza mara moja.

**Imetolewa na:**

**Suzan C. Mshakangoto**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
**Wizara ya Viwanda na Biashara**